

# JUKATA: Katiba mpya ipo njia panda

Na Irene Mark

JUKWAA la Katiba Tanzania (JUKATA) limesema mchakato wa kupata Katiba mpya upo njia panda hivyo hakuna uwezekano wa kupata Katiba mpya Aprili 26, 2014 kama ilivyotarajiwa.

Kwa sababu hiyo, limejiandaa kufanya marekebisho ya Katiba ya sasa kwenye vipengele vya uchaguzi ili kupisha chaguzi za

serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kuanza kwa mkutano wa waangalizi na wataalamu 200 wa michakato ya Katiba, Mwenyekiti wa Jukata, Deus Kibamba, alisema uwezekano wa taifa kupata Katiba mpya upo njia panda.

Alisema waangalizi hao wali-

fanya kazi nzuri Kenya na Zambia ambao wamepata Katiba bora hivyo ushauri wao utasaidia kuipitisha Tanzania kwenye kipindi hiki kigumu.

Kwa mujibu wa Kibamba kitendo cha wabunge kupigana ndani ya Bunge ni dalili za hofu kwa ajili ya masilahi zao na kwamba wanajadili mambo yasiyowahusu kitu kina-chowafanya sasa kulipeleka taifa

kwenye kuandika katiba tatu badala ya moja.

"Tunataka kujibu maswali magumu... ukiona ngumi za wabunge ujue mchakato upo njia panda, hakuna uhakika wa kupata Katiba mpya kwa wakati na huu mchakato hautakiwi kuburuzwa.

"Kinachofanyika ni kwa ajili ya Watanzania wote si wanasiasa, ndiyo maana tunashauri njia

muafaka ni kufanya mabadiliko makubwa ya Katiba kwenye kipengele cha uchaguzi.

Awali mwenyekiti huyo alisisitiza kwamba kilichotokea bungeni na kusababisha vurugu ni uongozi mbovu wa kiti cha spika.

Baadhi ya washiriki wa mkutano huo ni asasi ya Konrad Adenauer Stiftung (KAS) na Fredrich Ebert Stiftung (FES), maprofesa wa sheria na wanaharakati.